# KAULI YA SERIKALI KUHUSU HALI YA CHAKULA NCHINI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Na. 49 (1) na (2) na (3) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa kauli ya Serikali juu ya hali ya chakula nchini.

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba nchi yetu iko salama kwa upande wa chakula na hivyo hakuna wasiwasi wa hali tete ya kuwepo kwa njaa. Hali iiliyopo ni baadhi ya maeneo nchini kuwa na upungufu wa chakula na kupanda kwa bei ya mahindi ambapo wafanyabiashara nao wametumia fursa hii kuingia sokoni na kununua mahindi kwa bei ya juu.

Pamoja na changamoto hii, NFRA inayo akiba ya kutosha ambayo itaendelea kupelekwa kwenye maeneo yaliyobainika kuwa na uhaba, hivyo hakuna mwananchi atakayekufa kwa njaa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka mwaka 2011/2012, uzalishaji wa chakula nchini ulikuwa wa kuridhisha. Tathmini ya uvunaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2011/2012 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2012/2013, iliyofanywa mwezi Juni, 2012 ilionesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa ujumla katika msimu huo ulifikia tani milioni 13.6 zikiwemo tani milioni 7.6 za nafaka na tani milioni 6.0 za mazao yasiyo nafaka. Uzalishaji huo ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani milioni 12.0 kwa mwaka 2012/2013 na kuwepo kwa ziada ya tani milioni 1.6 za chakula. Hivyo nchi yetu inajitosheleza kwa asilimia 113.

## 2.0 HALI YA UPATIKANAJI WA CHAKULA MSIMU 2012/13

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa chakula imeendelea kuwa ya kuridhisha. Pamoja na hali ya chakula kwa ujumla kuwa ya kuridhisha, kuna baadhi ya maeneo yenye uhaba wa chakula kutokana na mvua kutonyesha vizuri katika maeneo yanayopata mvua za vuli na katika baadhi ya maeneo uhaba wa chakula umesababisha kupanda sana kwa bei za chakula katika maeneo husika.

Tathmini ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini imebaini kuwepo na ziada ya chakula katika mikoa 7 ya Iringa, Rukwa, Mbeya, Kagera, Mtwara, Kigoma na Ruvuma, utoshelevu katika mikoa 8 ya Morogoro, Pwani, Mara, Tanga, Lindi, Mwanza, Singida na Dodoma; na uhaba katika mikoa 6 ya Shinyanga, Tabora, Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Dar es Salaam.

Uzalishaji wa chakula nchini, hususan nafaka kwa msimu wa kilimo 2011/2012 ulifikia tani 7,558,342 wakati mahitaji yetu ni tani 7,551,244 na hivyo kujitosheleza na kuwa ziada ndogo ya tani 7,097 za nafaka. Ziada hii ni ndogo hivyo ni lazima itumike kwa uangalifu. Aidha, uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo ya nafaka (viazi, muhogo, ndizi, maharage, n.k.) unakadiriwa kuwa tani 6,014,463 wakati mahitaji ya Taifa ni tani 4,438,870 hivyo kuwa na ziada ya tani 1,575,592.

**Mheshimiwa Spika**, Tathmini imebainisha pia kuwepo kwa uhaba wa chakula katika Halmashauri 63 zilizo katika mikoa 17 katika viwango tofauti (Kiambatisho Na 1). Aidha, Halmashauri 35 katika mikoa 12 tayari zimeidhinishiwa na Kamati ya Maafa (TANDREC) jumla ya tani 18,417.8 za chakula cha msaada cha miezi 2-3 kwa kipindi cha Novemba, 2012-Januari, 2013) kwa ajili ya watu 526,607 walioainishwa kuwa na uhaba wa chakula wa kukithiri (Kiambatisho Na 2).

## 3.0 BEI ZA MAZAO

**Mheshimiwa Spika**, Bei ya mazao ya nafaka katika masoko makuu nchini bado iko juu. Kwa mfano, Uchambuzi wa bei za vyakula unaonyesha kuwa bei ya wastani ya mahindi kwa kilo kitaifa mwezi Septemba ilikuwa Sh. 540 wakati bei ya tarehe 15 Oktoba ilikuwa Sh. 570 kwa kilo.

Mwelekeo huu unaonesha kuwa bei inaendelea kupanda ikilinganishwa na miezi ya Juni hadi Septemba 2012. Hali hii inaashiria kupungua kwa kiasi cha mahindi kinachoingia sokoni wakati huu. Aidha, bei ya wastani ya mahindi kwa mwezi Septemba 2012 katika masoko ya miji mikuu ya mikoa 10 iko juu ya bei ya wastani wa kitaifa ya Sh. 540 kwa kilo. Baadhi ya masoko hayo ni Mwanza (Sh. 670), Tabora (Sh. 660), Musoma (Sh. 620), Bukoba (Sh. 610), Dar es Salaam (Sh. 600) na Shinyanga (Sh. 600). Aidha, bei ya wastani ya mchele kitaifa hivi sasa ni Sh. 1,640 kwa kilo.Hili ni ongezeko la asilimia 3.5 ikilinganishwa na bei ya mwezi Agosti au asilimia 21 ikilinganishwa na mwaka jana kipindi kama hiki.

## 4.0 HALI YA CHAKULA DUNIANI NA NCHI JIRANI

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) iliyotolewa mwezi Juni, 2012 inaonesha kuwa katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa nafaka duniani utaongezeka kwa asilimia 3.2. Jumla ya tani milioni 2,419 za nafaka zitazalishwa ikilinganishwa na matumizi ya nafaka ya tani milioni 2,376 kwa mwaka 2012/2013, matumizi ya nafaka kwa ajili ya chakula cha mifugo yataongezeka kwa asilimia 3.8 wakati matumizi ya chakula yanatazamiwa kuongeza kwa asilimia 1 na kiasi kikubwa kwenda sambamba na ukuaji wa watu duniani. Akiba ya nafaka duniani inatazamiwa kufikia tani millioni 36, ikiwa ni ongezeko kidogo kutoka kiwango cha mwaka jana.

Kutokana na ongezeko hilo, takriban nchi 66 duniani zilizo kwenye kundi la nchi maskini zenye kipato kidogo zinatazamiwa kunufaika na uzalishaji ulioongezeka na hivyo kupunguza kwa kiasi uagizaji wa nafaka kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ongezeko hilo, uzalishaji wa mazao ya chakula unatazamiwa kupungua na hivyo kusababisha Uhaba wa chakula kwa viwango mbalimbali kwa mwaka 2012/2013 katika takriban nchi 36 duniani hasa kutoka kundi la nchi maskini zenye kipato kidogo za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kwa ujumla nchi nyingi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika ni miongoni mwa nchi hizo ambapo baadhi ya nchi jirani hususan, Burundi, Congo (DRC), Kenya, Sudan ya Kusini, Somalia, Madagascar, Malawi na Msumbiji zinatazamiwa kuwa na maeneo yatakayokabiliwa na uhaba wa chakula kutokana na sababu mbalimbali hasa ukame, mafuriko na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Kutokana na Uhaba huo na ikizingatiwa kuwa nyingi ya nchi hizo zilikuwa na uhaba mkubwa wa chakula kwa mwaka jana, bei za nafaka katika maeneo hayo hususan Kenya, Uganda, Sudan ya Kusini zimeendelea kupanda kuanzia kipindi cha Januari hadi Mei 2012. Bei za juu zaidi zimeripotiwa katika masoko ya Juba, Kampala na Nairobi.

Kwa mfano, bei ya mtama katika soko la Juba, Sudani ya Kusini kwa mwezi Aprili, 2012 imepanda kwa asilimia 145 ikilinganishwa na ile ya mwaka jana kipindi kama hicho wakati bei ya mahindi Soko la Kampala kwa mwezi Mei, 2012 imepanda hadi kufikia dola za Kimarekani 390 kwa tani au shillingi 616,200 za Kitanzania kwa tani sawa na ongezeko la asilimia 40 ikilinganishwa na viwango vya mwezi Mei, 2011.

Aidha, kati ya mwezi Septemba na Oktoba, 2012 bei ya jumla husUsan ya mazao ya nafaka katika nchi jirani imepanda na kuchochea kwa kiwango kikubwa ongezeko la biashara ya mazao ya chakula kutoka nchini kwenda nchi hizo zenye uhaba wa chakula. Aidha, hali hiyo imechochea ongezeko kubwa la bei ya chakula katika masoko ya miji mikuu ya mikoa katika maeneo ya mipakani na hivyo kuathiri usalama wa chakula hasa kwa wananchi wa kipato cha chini wenye uwezo mdogo wa kujinunulia chakula.

## 5.0 HATUA ZINAZOCHUKULIWA NA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na hali ya uhaba wa chakula,hususan nafaka katika mwaka 2012/2013 na kuendelea kupanda kwa bei za vyakula, Serikali inachukua hatua zifuatazo;

i. Kuhamisha sehemu ya akiba ya nafaka iliyopo kwenye maghala yaliyopo Sumbawanga, Makambako na Songea kwenye ziada kwenda kwenye maghala ya Dar es Salaam, Dodoma, Shinyanga na Arusha yaliyo karibu na maeneo yenye uhaba wa chakula.

Hatua hiyo itaiwezesha Serikali kukabiliana na uhaba wa chakula na mahitaji mengine ya soko kwa haraka zaidi;

Hadi sasa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) ina akiba ya takribani tani 100,000 na inaendelea kununua nafaka kutoka kwa wakulima wa mikoa ile iliyozalisha ziada hususan, mikoa ya Rukwa, Iringa, Mbeya na Ruvuma;

ii. Kuhimiza wananchi kutumia aina mbalimbali za vyakula ikiwa ni pamoja na muhogo, viazi vitamu, viazi mviringo, ndizi na vyakula vingine ambavyo vinapatikana kwa wingi katika maeneo yao; na

iii. Serikali imeagiza mikoa na Halmashauri za wilaya zenye uhaba wa chakula kuongeza upatikanaji wa chakula katika maeneo yao kwa kuhamasisha wafanyabiashara wenye uwezo wa kununua chakula kutoka mikoa yenye ziada na kuuza kwenye maeneo yenye uhaba wa chakula.

iv. Wakulima wanashauriwa kutumia vizuri mvua zinazoanza kunyesha sasa kupanda mbegu za mazao yanayokomaa haraka. Tayari maandalizi muhimu ya msimu wa kilimo wa 2012/13 yamekamilika kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na kufikisha mbolea Wilayani na baadhi ya Vijiji.

v. Halmashauri zote zihakikishe kwamba skimu zote za umwagiliaji na mabonde yenye unyevu zinatumika kikamilifu na kuelekeza pembejeo muhimu za kilimo katika skimu hizo.

Serikali inawahimiza wananchi wote katika ngazi ya kaya hususan wakulima kuepuka matumizi mabaya ya chakula ikiwemo kutengeneza pombe na ikibidi wauze ziada tu ili kujiwekea akiba ya chakula cha kutosha kwa ajili ya mahitaji ya kaya zao mpaka msimu ujao.

## 6.0 USAMBAZAJI WA VOCHA NA PEMBEJEO ZA KILIMO MSIMU WA KILIMO WA 2012/2013

### 6.1 Ruzuku ya Pembejeo

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, jumla ya kaya 940,783 katika Mikoa 23 zitanufaika na ruzuku ya pembejeo kwa ajili ya mazao ya mahindi na mpunga ikilinganishwa na kaya 1,800,000 ambazo zilinufaika na ruzuku kwa mwaka 2001/2012.

Kati ya kaya hizo, kaya 640,783 zitatumia fedha za Serikali na kaya 300,000 zitatumia fedha za Benki ya Dunia (Kiambatisho Na. 3). Aidha, ruzuku ya mtama na alizeti itahusisha jumla ya tani 402 za mtama kwa ajili ya ekari 190,000 na tani 366 za alizeti kwa ajili ya ekari 90,000 ambazo zitatolewa kwa wakuilma wa mazao hayo.

Chini ya utaratibu huo, kila ekari moja ya mtama na alizeti itapata mfuko mmoja wa kilo 50 ya mbolea ya kupandia aina ya Minjingu Mazao ambapo jumla ya tani 14,000 za mbolea ya Minjingu Mazao zinatarajiwa kutumika.

### 6.2 Upatikanaji na Usambazaji wa mbegu bora

Hadi tarehe 19/10/2012, jumla ya tani 2,824.3 mbegu bora zikiwemo tani 2,814.3 mahindi na tani 10 za mpunga zilikuwa zimefikishwa kwenye Mikoa inayoanza msimu wa kilimo mapema ambayo mahitaji yake ni tani 2.232.6 (Kiambatisho Na. 4) . Makampuni ya mbegu yanaendelea kukamilisha uvunaji, usafirishaji na ufungashaji wa mbegu ili kuzipeleka mikoani. Mahitaji ya mbegu nchini ni tani 60,000. Tayari makampuni mawili yameshateuliwa kwa ajili ya upelekaji wa mbegu za mtama na alizeti kwa wakulima kuanzia tarehe 30 Oktoba, 2012.

### 6.3 Upatikanaji na Usambazaji wa mbolea

Hadi tarehe 30 Septemba, 2012 jumla ya tani 150,000 za mbolea kati ya mahitaji ya tani 400,000 zipo nchini. Jumla ya tani 85,495 za mbolea zinatarajiwa kuingizwa nchini ifikapo tarehe 30 Desemba, 2012. Aidha, jumla ya tani 18,977 kati ya tani 21,064 za mbolea ya Minjingu Mazao zinahitajika kwenye Mikoa inayotumia mbolea hii kwa kupandia zimekwishafikishwa katika maeneo ambayo msimu wa kilimo unaanza mapema (Kiambatisho Na. 5) na kiwanda cha Minjingu kinaendelea na upelekaji wa mbolea hiyo kwenye maeneo husika.

## 6.4 Upelekaji wa vocha maeneo ambayo msimu wa kilimo unawahi

Mikoa ambayo msimu wa kilimo unawahi imekwishapelekewa vocha ambazo hazikutumika mwaka 2011/2012. Jumla ya vocha 421,362 kati ya vocha 750,000 za mbegu na mbolea ya kupandia zinazotakiwa kugongwa mhuri zimepelekwa tarehe 27/8/2012 katika Mikoa ya Kigoma, Kagera,Geita, Mwanza, Mara, Shinyanga, Katavi (Wilaya ya Mpanda), Mbeya (Wilaya ya Rungwe na sehemu ya Wilaya za Ileje na Mbeya Vijijini), Morogoro (sehemu za Wilaya ya Mvomero) na Njombe (Wilaya ya Makete na sehemu ya Wilaya ya Njombe Vijijini). Zoezi la kugonga vocha mihuri limekamilika. Vocha zitapelekwa Mikoa ya Katavi (Wilaya ya Mlele na kaya zilizobakia kwa Wilaya ya Mpanda), Njombe (Wilaya za Ludewa, Wanging'ombe na Wilaya ya Njombe kwa kaya zilizobakia), Iringa, Mbeya (Wilaya za Mbozi na Wilaya ya Ileje kwa kaya zilizobajia).

## 6.5 Uchapaji wa vocha

Hadi tarehe 25/9/2012, Kampuni zilizoomba kuchapisha vocha zilikwishafanyiwa tathmini na taarifa ya tathmini hiyo kuwasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata maoni yao na hatimaye kibali cha ***No objection***. Benki ya Dunia walirudisha maoni ambayo yalifanyiwa kazi na kupelekwa tena tarehe 5/10/2012.

Baada ya mchakato wa maandalizi ya zabuni kuisha mzabuni aliyeshinda zabuni alipewa taarifa tarehe 18/10.2012. Chini ya utaratibu huu, vocha 2,072,349 zitachapishwa.

### 6.6 Makampuni kuteua Mawakala

Makampuni ya mbegu na mbolea yanaendelea na uteuzi wa mawakala wa pembejeo katika Mikoa. Aidha, Wizara imeyahimiza makampuni ya pembejeo kuweka kipaumbele kwenye Mikoa ambayo msimu wa kilimo unaanza mapema.

### 6.7 Waraka wa Usimamizi wa Utekelezaji wa Ruzuku kwa mwaka 2012/2012

Waraka wa Usimamizi wa Utekelezaji wa Ruzuku ya Pembejeo kwa mwaka 2012/2013 umekamilika na kutumwa Mikoa yote tarehe 25 Septemba, 2012. Waraka huo umewekwa kwenye tovuti ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika (*www.kilimo.go.tz*)

## 8.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Mikakati mingine ya baadaye itakayoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuimarisha usalama wa chakula ni pamoja na ifuatavyo:-

i. Ili kukabiliana na kupanda kwa bei za vyakula kunakochangiwa kwa kiasi kikubwa na uzalishaji mdogo na ukame Serikali itaendelea kuimarisha mikakati ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kuongeza uwekezaji katika kilimo na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia SAGCOT, ***Feed the Future, Bread Basket*****;** na kuongeza ruzuku ya pembejeo na mikopo ya zana bora za Kilimo.

ii. Kuhakikisha kwamba skimu zote za umwagiliaji na mabonde yenye unyevu zinasimamiwa ili zizalishe chakula kwa wingi na kila inapowezakana zaidi ya mara moja kwa mwaka.

iii. Serikali itaendelea kuijengea uwezo NFRA ili iweze kununua na kuhifadhi nafaka ya kutosha kukabiliana na maafa mbalimbali na kudhibiti bei za vyakula nyakati za uhaba. Lengo ni kununua tani 200,000 katika msimu wa ununuzi wa 2012/2013.

iv. NFRA itaendelea kuimarisha uwezo wake wa kuhifadhi kutoka uwezo wa sasa wa kuhifadhi tani 241,000 za chakula kwa kukarabati maghala yaliyopo na kujenga maghala mapya yenye uwezo wa kuhifadhi tani 160,000 ili hatimaye iweze kuhifadhi angalau tani 400,000 ifikapo 2015.

v. Serikali itaimarisha masoko (vituo) rasmi vya kuuzia mazao ili kudhibiti walanguzi wanaokwepa kununua mazao yaliyovunwa kwa kununua mazao yakiwa bado shambani. Hatua hii itasaidia, kumpa bei nzuri mkulima na Serikali kupata ushuru wa mazao unaostahili kwa kiasi cha mazao yanayouzwa ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Upungufu wa chakula unaoendelea katika nchi jirani hususan Burundi, Congo DRC,Kenya,Sudani Kusini, Somalia na nyingine na kwa kuzingatia kuwepo kwa fursa za kuzalisha mazao katika nchi yetu, Serikali itajikita zaidi katika kuzalisha mazao ya kutosha ili kupata ziada ya kuuza kwa kutumia fursa ya soko la mazao katika nchi jirani.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

**KIAMBATISHO NA.1 WILAYA 63 ZA MIKOA 17 ZENYE UHABA WA CHAKULA**

# Appendix 4: Vulnerable Areas 2012/13

**According to the 2011/12 Preliminary Forecast**

| S/N. | Region *(Ranked by extent of districts containing vulnerable areas)* | SSR Status | Districts (Number in list) | Districts *(Listed in order of dicreasing vulnerability)* |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shinyanga | | 7 | Bariadi, Kishapu, Meatu, Maswa, Kahama, Shinyanga M, Shinyanga (V) |
| 2 | Arusha | | 7 | Karatu, Monduli, Meru, Ngorongoro, Longido, Arusha MC, Arusha DC |
| 3 | Kilimanjaro | | 6 | Hai, Mwanga, Moshi DC, Moshi TC, Rombo, Same |
| 4 | Tabora | | 6 | Nzega, Igunga, Tabora (M), Uyui, Sikonge, Urambo |
| 5 | Dodoma | | 6 | Bahi, Chamwino, Dodoma (M), Kondoa, Kongwa, Mpwapwa |
| 6 | Tanga | | 6 | Tanga (M), Mkinga, Pangani, Korogwe( M), Korogwe (V), Handeni |
| 7 | Manyara | | 5 | Babati DC, Hanang, Kiteto, Mbulu, Simanjiro, |
| 8 | Singida | | 4 | Manyoni, Iramba, Singida (V), Singida (M) |
| 9 | Mwanza | | 3 | Magu, Kwimba, Misungwi |
| 10 | Coast | | 3 | Kibaha (M), Mafia, Rufiji |
| 11 | Mara | | 2 | Musoma V, Rorya, |
| 12 | Lindi | | 2 | Kilwa, Lindi |
| 13 | Morogoro | | 2 | Morogoro (V), Mvomero |
| 14 | Iringa | | 1 | Kilolo |
| 15 | Kagera | | 1 | Chato |
| 16 | Mbeya | | 1 | Mbozii |
| 17 | Mtwara | | 1 | Masasi |
| 18 | Dar es Salaam | * | - | |
| 19 | Kigoma | | - | |
| 20 | Rukwa | | - | |
| 21 | Ruvuma | | - | |
| | Total | | 63 | Total |
| | **TANZANIA:** Food Security Status: Self Sufficient (SSR=113%), Vulnerability 17 regions, 63 districts | **Regions** containing Vlnerable areas 17: 5 Deficit, 8 Self Sufficient, 4 Surplus | **Districts** containing Vulnerable areas 63: 31 deficit, 28 self sufficient, 4 Surplus | **In general,** While at national level Tanzania during 2012/13 will be 113% food self sufficient, 17 regions contain vulnerable areas in 63 districts….=>=> **Hence an early warning against likely misfortunes!!** |

**HALMASHAURI ZENYE MATATIZO YA UPUNGUFU WA CHAKULA NA LISHEMUHTASARI WA KITAIFA SEPTEMBA 2012** — Kiambatishi Na 2

| Mkoa | Halmashauri | Jumla ya Watu Wilayani | Idadi ya Watu Wenye Rasilimali Duni | % ya Watu Wenye Rasilimali Duni | Kaya Zenye Rasilimali Duni | Mgawanyo wa Watu kwa Makundi | | Kipindi cha Mahitaji | Jumla ya Mahitaji ya Chakula(MT) | Chakula cha Msaada | | | | Mahitaji ya Mbegu (MT) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Idadi ya Watu kwenye Phase 2 | Idadi ya Watu kwenye Phase 3 | | | Idadi ya Wenye Upungufu Mkubwa wa Chakula | Mahitaji ya Chakula cha Bure(MT) | Wenye Upungufu wa Wastani | Mahitaji ya Chakula cha Bei Nafuu (MT) | |
| Arusha | Karatu | 255,484 | 4,677 | 2 | 3,150 | 2,011 | | 2 | 48.3 | 201 | 4.8 | 1,810 | 43.4 | 9.4 |
| Arusha | Longido | 70,682 | 18,940 | 27 | 12,001 | | 12,311 | 2 | 295.5 | 1,231 | 29.5 | 11,080 | 265.9 | 37.9 |
| Arusha | Monduli | 181,754 | 27,384 | 15 | 16,867 | 19,169 | | 2 | 460.1 | 1,917 | 46.0 | 17,252 | 414.0 | 54.8 |
| Arusha | Ngorongoro | 177,325 | 10,386 | 6 | 11,908 | 6,543 | | 2 | 157.0 | 654 | 15.7 | 5,889 | 141.3 | 20.8 |
| **Jumla** | | **685,245** | **61,387** | **9** | **43,926** | **27,723** | **12,311** | **2** | **960.8** | **4,003** | **96.1** | **36,030** | **864.7** | **122.8** |
| Dodoma | Bahi | 236,778 | 4,003 | 2 | 3,905 | 3,722 | | 3 | 134.0 | 372 | 13.4 | 3,350 | 120.6 | 7.0 |
| Dodoma | Chamwino | 301,353 | 12,925 | 4 | 15,311 | 11,115 | | 3 | 400.2 | 1,112 | 40.0 | 10,004 | 360.1 | 21.5 |
| **Jumla** | | **538,131** | **16,927** | **3** | **19,216** | **14,838** | | **3** | **534.2** | **1,484** | **53.4** | **13,354** | **480.7** | **28.5** |
| Kilimanjaro | Hai | 174,471 | 5,475 | 3 | 4,619 | | 2,738 | 2 | 65.7 | 274 | 6.6 | 2,464 | 59.1 | 11.0 |
| Kilimanjaro | Mwanga | 146,631 | 6,093 | 4 | 7,175 | | 2,437 | 2 | 58.5 | 244 | 5.8 | 2,194 | 52.6 | 12.2 |
| Kilimanjaro | Same | 270,388 | 37,802 | 14 | 26,724 | 5,670 | | 2 | 136.1 | 567 | 13.6 | 5,103 | 122.5 | 63.0 |
| **Jumla** | | **591,490** | **49,371** | **8** | **38,518** | **5,670** | **5,175** | **2** | **260.3** | **1,085** | **26.0** | **9760.9** | **234.3** | **86.1** |
| Lindi | Lindi (DC) | 476,892 | 8,078 | 2 | 7,033 | 2,423 | | 3 | 87.2 | 242 | 8.7 | 2,181 | 78.5 | 13.5 |
| **Jumla** | | **476,892** | **8,078** | **2** | **7,033** | **2,423** | | **3** | **87.2** | **242** | **8.7** | **2181.1** | **78.5** | **13.5** |
| Mara | Musoma (DC | 460,403 | 22,157 | 5 | 17,778 | 18,579 | | 2 | 445.9 | 1,858 | 44.6 | 16,721 | 401.3 | 3.1 |
| Mara | Rorya | 302,012 | 16,420 | 5.4 | 14,842 | 13,957 | | 2 | 335.0 | 1,396 | 122.7 | 12,561 | 1,104.1 | 73.7 |
| **Jumla** | | **762,415** | **38,577** | **5** | **32,620** | **32,535** | | **2** | **780.8** | **3,254** | **167.3** | **29281.8** | **1,505.4** | **76.8** |
| Manyara | Babati (DC) | 319,695 | 12,132 | 4 | 13,650 | | 9,798 | 3 | 371.2 | 1,031 | 37.1 | 9,281 | 334.1 | 24.3 |
| Manyara | Mbulu | 355,912 | 6,582 | 2 | 5,469 | | 5,606 | 3 | 201.8 | 561 | 20.2 | 5,046 | 181.6 | 13.2 |
| Manyara | Simanjiro | 212,860 | 32,288 | 15 | 21,692 | 27,445 | | 3 | 988.0 | 2,744 | 98.8 | 24,700 | 889.2 | 53.8 |
| **Jumla** | | **888,467** | **51,002** | **6** | **40,811** | **27,445** | **15,404** | **3** | **1,561.1** | **4,336** | **156.1** | **39026.6** | **1,405.0** | **91.2** |
| Morogoro | Morogoro (D | 313,745 | 3,885 | 1 | 6,156 | 2,603 | | 2 | 62.5 | 260 | 6.2 | 2,342 | 56.2 | 7.8 |
| Morogoro | Mvomero | 320,292 | 3,561 | 1 | 5,035 | 3,276 | | 2 | 78.6 | 328 | 7.9 | 2,948 | 70.8 | 7.1 |
| **Jumla** | | **634,037** | **7,445** | **1** | **11,191** | **5,879** | | **2** | **141.1** | **588** | **14.1** | **5291** | **127.0** | **14.9** |
| Mwanza | Kwimba | 407,737 | 55,341 | 14 | 23,789 | | 52,574 | 2 | 1,261.8 | 5,257 | 126.2 | 47,317 | 1,135.6 | 110.7 |
| Mwanza | Magu | 545,232 | 57,960 | 11 | 30,926 | 46,368 | | 2 | 1,112.8 | 4,637 | 111.3 | 41,731 | 1,001.6 | 115.9 |
| **Jumla** | | **952,969** | **113,302** | **12** | **54,715** | **46,368** | **52,574** | **2** | **2,374.6** | **9,894** | **237.5** | **89,048** | **2,137.2** | **226.6** |
| Shinyanga | Bariadi | 925,234 | 85,664 | 9 | 29,398 | 69,388 | | 4 | 3,330.6 | 6,939 | 333.1 | 62,449 | 2,997.6 | 171.3 |
| Shinyanga | Kahama | 919,795 | 37,259 | 4 | 40,330 | 23,101 | | 4 | 1,108.8 | 2,310 | 110.9 | 20,791 | 998.0 | 74.5 |
| Shinyanga | Kishapu | 367,425 | 75,347 | 21 | 26,106 | | 37,674 | 4 | 1,808.3 | 3,767 | 180.8 | 33,906 | 1,627.5 | 150.7 |
| Shinyanga | Maswa | 470,437 | 59,955 | 13 | 25,402 | 52,161 | | 4 | 2,503.7 | 5,216 | 250.4 | 46,945 | 2,253.3 | 119.9 |
| Shinyanga | Meatu | 381,570 | 39,969 | 10 | 12,201 | 13,190 | | 4 | 633.1 | 1,319 | 63.3 | 11,871 | 569.8 | 79.9 |
| Shinyanga | Shinyanga ( | 417,264 | 11,285 | 3 | 30,055 | | 6,545 | 4 | 314.2 | 655 | 31.4 | 5,891 | 282.7 | 22.6 |
| Shinyanga | Shinyanga ( | 232,246 | 7,518 | 3 | 3,449 | 3,007 | | 4 | 144.3 | 301 | 14.4 | 2,706 | 129.9 | 15.0 |
| **Jumla** | | **3,713,971** | **316,997** | **9** | **166,941** | **160,846** | **44,219** | **4** | **9,843.1** | **20,506** | **984.3** | **184,558** | **8,858.8** | **634.0** |
| Singida | Iramba | 481,437 | 20,593 | 4 | 20,074 | 11,738 | | 2 | 281.7 | 1,174 | 28.2 | 10,564 | 253.5 | 41.2 |
| Singida | Manyoni | 285,868 | 7,634 | 3 | 11,041 | 4,351 | | 2 | 104.4 | 435 | 10.4 | 3,916 | 94.0 | 15.3 |
| **Jumla** | | **767,305** | **28,226** | **4** | **31,115** | **16,089** | | **2** | **386.1** | **1,609** | **38.6** | **14,480** | **347.5** | **56.5** |
| Tabora | Igunga | 452,282 | 28,339 | 6 | 19,140 | 19,554 | | 2 | 469.3 | 1,955 | 46.9 | 17,599 | 422.4 | 56.7 |
| Tabora | Nzega | 582,583 | 13,093 | 2 | 10,210 | 9,034 | | 2 | 216.8 | 903 | 21.7 | 8,131 | 195.1 | 26.2 |
| Tabora | Sikonge | 186,459 | 8,173 | 4 | 4,671 | 5,640 | | 2 | 135.3 | 564 | 13.5 | 5,076 | 121.8 | 16.3 |
| Tabora | Uyui | 372,758 | 11,186 | 3 | 5,571 | 9,829 | | 3 | 353.9 | 983 | 35.4 | 8,847 | 318.5 | 28.5 |
| **Jumla** | | **1,594,082** | **60,791** | **4** | **39,592** | **44,058** | | **2** | **1,175.3** | **4,406** | **117.5** | **39,652** | **1,057.8** | **127.7** |
| Tanga | Korogwe | 338,302 | 21,177 | 6 | 25,791 | 4,659 | | 2 | 111.8 | 466 | 11.2 | 4,193 | 100.6 | 9.3 |
| Tanga | Lushoto | 527,845 | 15,430 | 3 | 15,137 | 3,395 | | 2 | 81.5 | 339 | 8.1 | 3,055 | 73.3 | 5.6 |
| Tanga | Pangani | 57,827 | 6,241 | 11 | 5,114 | 4,992 | | 2 | 119.8 | 499 | 12.0 | 4,493 | 107.8 | 8.3 |
| **Jumla** | | **923,974** | **42,847** | **5** | **46,042** | **13,046** | | **2** | **313.1** | **1,305** | **31.3** | **11,741** | **281.8** | **23.2** |
| **Jumla Kuu** | | **12,528,979** | **794,951** | **6** | **531,720** | **396,920** | **129,683** | **2** | **18,417.8** | **52,712** | **1,931.0** | **474,405** | **17,378.6** | **1,501.8** |

**CHANZO:** TATHMINI YA KINA YA HALI YA CHAKULA NA LISHE SEPTEMBA 2012